

**HOTUBA YA MHE. DR. VINCENT ANNEY NAANO, MKUU WA**  
**WILAYA YA MUSOMA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA**  
**SIKU YA MAZINGIRA AFRIKA TAREHE 3 MACHI, 2017 KATIKA**  
**SHULE YA SEKONDARI KIARA**

Wahe. Madiwani mliopo hapa,  
Mkurugenzi wa Manispaa,  
Wakuu wa Idara na Vitengo,  
Watendaji  
Wenyeviti wa mitaa  
Walimu  
Jumuiya ya shule  
Wanafunzi  
Mabibi na Mabwana.

**Ndugu wananchi**

Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai leo na kuendeleza mapambano ya kupigania maendeleo ya nchi yetu.

Maendeleo yanayohitajika Duniani kote leo hususan nchi yetu ni "**Maendeleo endelevu**"(sustainable development) ambayo maana yake ni "maendeleo yanayomwezesha binadamu wa kizazi cha leo kupata mahitaji yake, bila kuathiri uwezekano wa vizazi vijavyo kupata mahitaji yao". Kamwe hatuwezi kufikia lengo la maendeleo endelevu bila kutunza mazingira yetu. Hii ina maana kuwa, kwa vile mazingira ndicho kikapu kinachohifadhi mahitaji yote ya binadamu (hewa, maji mwanga, chakula, nishati, mandhari, dawa, mvua, rutuba kwenye udongo n.k), ni lazima binadamu afanye shughuli zake za kimaendeleo katika Nyanja zote za maisha akitumia rasilimali kutoka kwenye mazingira kwa werevu mkubwa na uadilifu, nidhamu na uungwana kwa vizazi vitakavyofuata baada yake ili vizazi hivyo vikute mahitaji yao yote yakipatikana kwenye mazingira sawa na/au zaidi ya mahitaji yaliyopo leo katika mazingira. Katika maana pana ya sayansi ya utunzaji wa mazingira zana hii ya muhimu inaitwa haki sawa baina ya vizazi (inter-generational equity).

**Ndugu wananchi**

Leo tunaadhimisha Siku ya Mazingira Afrika tukiwa na lengo kuu la kupeana hamasa ya kutunza mazingira yetu, kufanya vitendo vya kuyalinda

mazingira na kukemea matendo yanayopelekea uharibifu wa mazingira. Katika halmashauri yetu ya Manispaa ya Musoma tangu tarehe 1 Machi, 2017 hadi leo tarehe 3 Machi, 2017 tumegawa jumla ya miche ya miti ipatayo.....ambayo imepandwa maeneo mbalimbali.

Natoa wito kwa wananchi wote wa halmashauri ya manispaa ya Musoma kuitikia kwa moyo mmoja zoezi la upandaji miti. Kila kaya ipande miti isiyopungua mitatu (3) na kuisimamia hadi ikue. Kipaumbele kiwe kupanda miti ya matunda na mbao ili kuleta tija kubwa zaidi. Wapo wadau wengi katika halmashauri yetu ambao wanaotesha miche na kuuza kwa bei nafuu sana.

Aidha naagiza kila shule ipande miti katika maeneo ya shule. Manispaa yetu ina jumla ya wanafunzi **42,202** wa shule za msingi na wanafunzi **12,557** wa shule za sekondari. Jumla ni wanafunzi **54,759**. Naagiza kila mwanafunzi apande na kutunza mti mmoja tu. Kupitia hatua hiyo tutakuwa tumepanda miti **54,759**. Jambo hili lianze sasa, Afisa Elimu Msingi na Afisa Elimu Sekondari simamieni jambo hili kwa ushirikiano na walimu wenu. Tunataka kuona shule zote zinageuka kuwa za kijani. Kufanya hivyo kutasaidia kupunguza kukua kwa hali ya jangwa na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

### **Ndugu wananchi**

Sambamba na hilo, tuweni mabalozi wa kukemea uharibifu wa mzingira: Utupaji ovyo wa taka, uvuvi haramu, utiririshaji wa maji taka, uchomaji moto misitu, biahara ya wanyama pori hususan wanyama walio katika hatari ya kutoweka kama tembo, kilimo kisicho endelevu, uharibifu wa vyanzo vyta maji na ukataji miti ovyo.

Naomba pia shule zote zianzishe klabu za mazingira za wanafunzi ambapo wanafunzi watakuwa na makundi ya kupeana elimu ya kutunza mazingira na kuwa chachu kwa wanafunzi wenzao na jamii kwa ujumla. Ofisi ya Afsa Mazingira iweke mpango wa kutembelea shule kutoa elimu ya mazingira kwa klabu na wanafunzi.

Mwisho kabisa, Nawashukuru sana kwa namna mlivyohiari kushiriki katika zoezi hili la leo. Tukumbuke suala la kutunza mazingira ni jambo la kila siku na linagusa nyanja zote na idara zote. Mazingira ni suala mtambuka. Kila mmoja wetu ni mdau muhimu wa Mazingira.

Tutunze Mazingira Yatutunze.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Manispaa yetu ya Musoma, Mungu ibariki Kiara Sekondari.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**